Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

Swaum Ya Mwezi Wa Ramadhaan Kama alivyotekeleza Mtume (صلى الله عليه وسلم)

[Sheikh Ali al-Halabi na Sheikh Saleem al-Hilaali]

10th Ramadhaan 1431
20th August, 2010

Volume 1, Issue 3

[Endelea kutoka Vol 1, Issue 2]

Amesema ((رب العزّة Mola wa Utukufu na Nguvu:

"Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allaah."

Kwahivyo, milango ya motoni hufungwa na milango ya peponi hufunguliwa kwani vitendo vizuri huwa vyengi na maneno mazuri huenea kila mahali. Akasema Mtume: (صلى الله عليه وسلم)

"Unapoingia mwezi wa Ramadhaan, milango ya peponi hufunguliwa na milango ya motoni hufungwa na mashetani hufungwa kwa minyororo."

Yote haya hufanyika katika usiku wa kwanza wa mwezi uliobarikiwa kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم)

"Unapoingia usiku wa kwanza wa mwezi wa Ramadhaan, Majini waovu hufungwa. Milango ya moto hufungwa - usifunguliwe mlango hata mmoja, na hufunguliwa milango ya pepo, usifungwe hata mlango mmoja miongoni mwa milango ya pepo; Akanadi mwenye kunadi miongoni mwa viumbe bora katika viumbe vya Allaah: "Ewe mwenye kutaka kheri njoo, na Ewe mwenye kutaka shari komeka." Na kuna wengi ambao Allaah anawawacha huru na Moto. Na hilo ni katika kila usiku."

- **LAILATUL-QADR (USIKU ULIOBARIKIWA)**

Ushajionea, ewe mja mu'min, vipi Allaah (جل جلاله) alivyouchagua mwezi wa Ramadhaan, kwani Qur'aan Tukufu iliteremshwa katika mwezi huo, na kutokana na nukta hii mambo mengine huwenda yakafahamika vyema:

Siku iliyo bora zaidi mbele ya Allaah iko katika mwezi ambao Alipoiteremsha Qur'aan, kwahivyo (siku hiyo) inapasa kuwa na mambo makhsusi kwa kufanya amali za ziyada. Jambo hili limeshuhudiwa na yaliyopokewa kuhusu kuutafuta (huo usiku wa) *Lailatul-Qadr* na kujitahidi kufanya vitendo vya ziyada uingiapo wakati huo, na haya yatakuja *Insha-Allaah*, katika mlango kuhusu *Lailatul-Qadr*.

Yakwamba baraka iliyowajilia Waislamu mara nyingi husababisha kuongezeka amali za kumshukuru Allaah, na limeshuhudiwa hili na maneno yake Muumba baada ya kutaja kuhusu ukamilifu wa ne'ema za mwezi wa Saumu:

"(Aliwataka nyinyi) mulazimike kukamilisha idadi maalum (ya masiku), na kwamba mumshukuru Allaah kwa kuwaongoza ili mupate kumshukuru."

Na maneno yake (تبـارك وتعالى) baada ya kutaja kukamilika kwa ne'ema ya Hajj:

"Na mwishapo kuzitimiliza Ibaada zenu (za Hijja), basi mtajeni Allaah kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu; bali mtajeni zaidi (Allaah)."

Kuwajibika Kufunga Katika Mwezi Wa Ramadhaan

- **Na atakaefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake**

Kutokana na fadhla zilizotangulia kutajwa, Allaah (سبحانه وتعالى):

Alifaradhisha kwa Waislamu kufunga katika mwezi wa Ramadhaan. Hatahivyo, kwa vile ni jambo gumu sana kuiachisha nafsi matamaniwa yake na kuiepusha na yale mambo ambayo huyaona kuwa na ushawishi, saumu haikufaradhishwa mpaka mwaka wa pili wa Hijrah. Basi nyoyo zilipojengeka juu ya Tawheed na juu ya kuyatukuza yale aliyoyafaradhisha Allaah, ndipo kisha wakaongozwa kwenye hilo (la kufunga) hatua baada ya hatua. Mwanzoni walikhiyarishwa na ikawa ni bora kwao wao kufunga. Kwa vile lilikuwa ni jambo gumu sana kwa maswahaba (رضي الله عنه,) yoyote aliyetaka kuwacha kufunga na badala yake amlishe masikini aliweza kufanya hivyo. Amesema Aliye Mpole na Mwenye Huruma (الرؤف الرحيم) :

"Na wale wasioweza, watoe fidia kwa kumlisha masikini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake. Na (huku) kufunga ni bora kwenu. Ikiwa mnajua (haya basi sasa fuateni).

- **Atakaekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhaan) afunge**

Kisha Aayah iliyofuatia ikateremshwa, na ikaifuta aayah hii. Kama tulivyoambiwa na maswahaba wawili watukufu, 'Abdullaah Ibn 'Umar na Salamah Ibn al-Akwa (رضي الله عنهم), wote wawili walisema, '*Imefutwa na:*

"(Mwezi huo mulioambiwa mufunge) ni mwezi wa Ramadhaan ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo hii Qur'aan ili iwe uwongozi kwa watu, na hoja zilizo wazi wa uwongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili). Atakaekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhaan) afunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi (atimize) hisabu (ya siku alizowacha kufunga) katika siku nyingine. Allaah Anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na pia (anakutakieni) mutimize hisabu hiyo, na (anakutakieni) kumtukuza Allaah kwa kuwa amekuongozeni, ili mupate kushukuru."

Ibn Abee Laylaa amesema: *"Maswahaba wa Muhammad* (صلى الله عليه وسلم) *wametuhadithia: yakwamba waliteremshiwa Ramadhaan na ikawa ni nzito kwao. Kwahivyo wale ambao hawakufunga waliwalisha masikini kwa kila siku aliyowacha mtu kufunga, na hii ilikuwa ni ruhusa kwao, lakini kisha hukmu hii ikaondolewa na (Aayah isemayo)*

"Na (huku) kufunga ni bora kwenu ikiwa mnajua".

Na wakaamrishwa kufunga.

Kisha, kufunga mwezi wa Ramadhaan ikawa ni mojawapo ya misingi ya Uislamu na nguzo za Dini, kutokana na maneno yake Mtume wa Rehma na uongofu (صلى الله عليه

(Endelea katika Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

Swaum	1-3
Mwezi Kongo	3
Matangazo	3
Ukumbi wa Kina mama	4

Nukta Muhimu za Mazingatio:

1. Kutakuwa na Darsa za wanawake katika mwezi wa Ramadhaan, msikiti wa Mazrui, kuanzia saa Nne asubuhi mpaka Adhuhuri—kila siku isipokuwa Ijumaa.
2. Jipatie Cd za Ustadh Na'maan kuhusu jinsi Älivyokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifunga mwezi wa Ramadhaan. Na pia Cd za Mawaidha mbalimbali za ma-Duáat wetu.
3. Jipatie nakala ya vitabu vifuatavyo:

- Tafsiri ya Soorah Qaaf. [Sh. Nassor Khamis]
- Namna Ya Swala Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). [Sh. Al-Albaani]
- Damu Asilia Za Wanawake. [Sh. Ibn Uthaymeen]
- Na Risala nyenginezo zenye faida katika Dini.

Utayapata Yote hayo katika Maktaba ya QSS—Mombasa.

...Swaum Ya Mwezi wa Ramadhaan

(Continued from page 1)

وسلم) aliposema:"*Umejengwa Uislamu juu ya mambo matano: Kushuhudia yakwamba hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kwenda kuhiji katika Nyumba, na kufunga mwezi wa Ramadhaan.*

Kuhimizwa Kufunga Katika Mwezi Wa Ramadhaan

- **Kusamehewa Madhambi**

Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametusisitiza kila mmoja wetu afunge katika mwezi wa Ramadhaan, akabainisha ubora wake na daraja yake iliyo juu kabisa, kiasi cha kwamba lau kama iwapo mwenye kufunga ana madhambi mengi kiasi cha povu lililoko juu ya bahari, basi yatakuwa ni yenye kusamehewa kutokana na kitendo hiki kizuri kilicho barikiwa.

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه), kutoka kwa Mtume ((صلى الله عليه وسلم) aliyesema: "*Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhaan, kutokana na Eemaan na akitarajia malipo mema (kutoka kwa Allaah), basi atasamehewa madhambi yake yaliyopita.*"

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "*Swala tano, na ijumaa mpaka ijumaa, na Ramadhaan mpaka Ramadhaan, ni kafara ya kufutiwa madhambi yaliyowahi kutokea katikati, endapo mtu atajiepusha na madhambi makubwa.*"

Akapokea tena Abu Hurairah ((رضي الله عنه) yakwamba: "*Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipanda juu ya mimbar akasema: Aameen, Aameen, Aameen. Ikasemwa, "Ewe mtume wa Allaah, ulipanda juu ya mimbar kisha ukasema 'Aameen, Aameen, Aameen'?" akasema, "kwa hakika Jibraa'eel 'Alayhis-salaam alinijia akasema, "yoyote ambae aliyeufikia mwezi wa Ramadhaan na isiwe ni sababu ya kusamehewa (madhambi yake) na akaingia motoni, basi Allaah na amuweke mbali, sema 'Aameen', ndio na mimi nikasema: "Aameen"... Hadeeth*

- **Yakwamba maombi (du'a') hutakabaliwa na kuachwa huru na moto huidhinishwa**

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Katika kila usiku na mchana wa mwezi wa Ramadhaan, kuna watu ambao Allaah huwawacha huru na moto, na kwa kila Muislamu kuna du'aa' awezayo kuiomba na kutakabaliwa.*

- **Atakuwa ni miongoni mwa wafuasi wa kihakika wa Mitume na mashahidi**

Kutoka kwa 'Amr Ibn Murrah al-Juhanee (رضي الله عنه) aliyesema: "*Alikuja mtu mmoja kwa Mtume ((صلى الله عليه وسلم akasema: "Ewe mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) je iwapo mimi nitashuhudia yakwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba wewe ni Mtume wa Allaah, nikaswali swala tano, na nikatoa Zakaah, na nikafunga na kusimama kwa ajili ya kuswali katika mwezi wa Ramadhaan, hapo mimi nitakuwa ni miongoni mwa watu gani?" Akasema: "Utakuwa ni miongoni mwa wafuasi wa kweli wa mitume na mashahidi.*"

- **Onyo Kali Dhidi Ya Kuacha Kufunga Mwezi Wa Ramadhaan Kwa Kusudi**

Abu Umaamah al-Baahilee (رضي الله عنه) amesema: "Nimemsikiya Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Nilipokuwa nimelala, watu wawili walinijia wakanishika mikono yangu na kunichukuwa mpaka kwenye mlima wenye muinuko mkali wakaniambia: 'Haya panda hapo', nikawajibu, 'mimi siwezi kupanda hapo.' Wakasema: 'Sisi tutakurahisishia.' Basi nikapanda mpaka nikafika kwenye kilele cha mlima huo ambapo nikaanza kusikia sauti ya kilio cha kutisha, nikasema: 'Ni kelele gani hizo?' Wakanijibu, 'hayo ni makelele ya watu wa motoni.' Kisha wakanichukuwa mbele zaidi mpaka nikawafikia watu wametundikwa kwa shingo zao mifupa yao ya taya (skulls) imevunjika na kuturuzika damu nyingi, kisha nikasema: 'Na hawa ni kina nani?' akanijibu, 'Ni wale wenye kufunguwa saumu zao kabla ya wakati unaowapasa kufanya hivyo.'"

Amma kuhusu yaliyonukuliwa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم yakuwa alisema: "*Mwenye kuacha kufunga katika siku moja ya Ramadhaan kwa kusudia – hata kama atafunga milele, haitoweza kuifidia siku hiyo.*"

Hadeeth hii ni dha'eef, si swaheeh, kama tutakavyoichambua baadae kwa utondoti katika kitabu hichi, *Insha-Allaah.*

Hukmu Za Saumu

Jua na kutanabahi! Ewe Muislamu, Ewe mja wa Allaah, Allaah Atuzidishie sote 'Ilmu, jua yakwamba malipo haya mkubwa na faida nyingi zisizoweza kuhesabiwa isipokuwa na Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Rehma, hakuna atakaezipata isipokuwa yule mwenye kufunga Ramadhaan kulingana na aliyoyathibitisha Mtume wa mwisho (صلى الله عليه وسلم) katika Sunnah kwa ufafanuzi – kuziunganisha hukmu hizo na uwajibikaji huu mkubwa na mwezi huu uliobarikiwa.

Hapa tutazifafanua: bila ya kufuata rai ki-upofu zisizokuwa na dalili zozote, bali kuchukuwa kutoka katika Qur'aan Takatifu, na yaliyo swaheeh na hasan kutoka katika Sunnah zilizotwahirika – zilizofahamika kulingana na ufahamu wa wema wetu waliotutangulia, ma-Imaam wanne, na wale waliokuwa kabla yao – Maswahaba na waliofuata njia zao, na hii ni dalili yenye kukutosha wewe. Kutokana na maoni nya wanavyuoni, sisi tumechagua yaliyo sawa na bora katika misemo yao.

Inapokurubia Ramadhaan

- **Kuhesabu Siku Za Sha'baan**

Ummah wa Ki-Islamu unatakiwa kuanza kuzihesabu siku kuanzia mwanzoni mwa Sha'baan ili kujiandaa kwa Ramadhaan, kwani mwezi wowote ni Imma siku ishirini na tisa au thalathini. Kwahivyo, ikiwa mwezi kongo utaonekana, itambidi mtu afunge, na iwapo hilo halitowezekana kutokana na kutanda mawingu, basi itabidi siku thalathini za Sha'baan zikamilishwe. Allaah, Muanzilishi wa mbingu na Ardhi aliufanya muandamo wa mwezi kongo kuwa ni alama kwa watu ili waweze kuhesabu miaka, miezi, na masiku, na wala mwezi hauwezi kuzidi siku thalathini.

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه), yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema:

"Fungeni mutakapouona (mwezi) na fungueni mutakapouona; na iwapo utafichamana na mawingu, basi kamilisheni siku thalathini za Sha'baan."

Kutoka kwa Abdullaah Ibn 'Umar (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "*Musifunge mpaka muuone mwezi kongo na musifungue mpaka muuone, na iwapo utafichamana kwa mawingu, basi hesabuni (masiku ya Sha'baan)*."

Kutoka kwa 'Adiyy Ibn Haatim (رضي الله عنه), yakwamba Mtumen (صلى الله عليه وسلم) alisema:

"Pindi ikiwajia Ramadhaan basi fungeni (siku) thalathini isipokuwa iwapo mutauona mwezi kongo kabla ya hapo."

- **Mwenye Kufunga Katika Siku Ya Shaka Amemu'asi Abul-Qaasim (صلى الله عليه وسلم)**

Kwahivyo, haifai kwa Muislamu kuutanguliza mwezi wa Ramadhaan kwa kufunga siku moja au siku mbili kabla yake, akidhania yakwamba huwenda ikawa Ramadhaan ishaingia, isipokuwa hayo yakitokea katika siku zake za kawaida alizozoea kufunga.

Kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Musiitangulize Ramadhaan kwa kufunga siku moja au mbili kabla yake, isipokuwa mtu mwenye kufunga saumu yake ya kawaida – basi muacheni huyo aifunge.*

Kwahivyo tahadhari, Ewe Muislamu, yakwamba mwenye kufunga katika siku ambayo iliyo na shaka atakuwa amemu'asi Rasoolullaah (صلى الله عليه وسلم.) Silah Ibn Zufar amepokea kutoka kwa 'Ammaar yakwamba: "*Mwenye kufunga katika siku ambayo ina shaka amemu'asi Abul-Qaasim* (صلى الله عليه وسلم.)

Atakapoushuhudia (mwezi kongo) mmoja wenu fungeni na mufungue

(Continued on page 3)

Kujitokeza kwa mwezi kongo huthibitishwa kwa kupatikana ushahidi wa Waislamu wawili waadilifu, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم):*"Fungeni mutakapouona, na fungueni mutakapouona na tekelezeni nguzo za Hijjah kwa kutegemea hivyo na lau utafichikana kwa mawingu basi kamilisheni (siku) thalathini, na iwapo mashahidi wawili wakishuhudilia basi fungeni na fungueni."*

Hapatokuwa na mapenyo yoyote yakwamba ati kwa vile mashahidi wawili ndiwo watakao kubaliwa katika hali moja imaanishe yakwamba shahidi mmoja hatoweza kukubaliwa, bali ushahidi wa mtu mmoja yakwamba ameuona mwezi kongo pia unakubalika, kwani imethubutu yakwamba Ibn 'Umar ((رضي الله عنه amesema: *"Watu walijitokeza kuuangalia mwezi kongo, basi mimi nikampasha habari Mtume* ((صلى الله عليه وسلم*yakwamba mimi nimeuona, kwahivyo akafunga na kuwaamrisha watu wafunge.*

Kuazimiya (An-Niyyah)

- · **Uwajibikaji wa kuwa na niya ya saumu ya faradhi kabla ya mapambazuko ya alfajiri ya kweli**

Itakapothubutu yakwamba mwezi wa Ramadhaan umeanza, emma kwa kuushuhudia mwezi au kwa kutokana na ushahidi wa mtu fulani, kwa njia ya ukamilishaji wa idadi (*yaani*; siku thalathini za Sha'baan) hapo itamlazimu kila Muislamu anayewajibika chini ya Sharee'ah atie niya kufunga mpaka usiku, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mtu asiyeamua kufunga kabla haijaingia Fajr, basi atakuwa hana saumu."

Pia akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mtu asiyetia niya ya kufunga wakati wa usiku, basi atakuwa hana saumu".*

Mahali pa niya ni moyoni, kuitamka kwa ulimi ni jambo la uzushi (bid'ah) na upotofu – hata kama watu hulidhania jambo hilo kuwa ni zuri. Haja ya kuwa na niya tangu usiku ni makhsusi kwa saumu za faradhi kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akimjilia 'Aa'ishah ((رضي الله عنهاkatika masiku yasiyokuwa Ramadhaan na akimwambia: *"Una chakula chochote? Kama huna basi mimi nimefunga."*

Na imethubutu mfano wa hayo kutokana na vitendo vya Maswahaba: Abud-Dardaa', Abu Talhah, Abu Hurairah, Ibn 'Abbaas na Hudhaifah Ibn al-Yamaan (رضي الله عنهم)na twamuomba Allaah atufufue pamoja nao tukiwa chini ya bendera ya Mtukufu wa watoto wa Aadam (صلى الله عليه وسلم). Kwahivyo hii inahusiana na saumu za Sunnah na inaonyesha yakwamba uwaajibikaji wa kutia niya kabla ya mapambazuko ya alfajiri ya kweli ni kwa saumu za faradhi – na Allaah (سبحانه وتعالى) ndiye Mjuzi Bora.

- **Uwajibikaji na mahitaji yanategemea uwezo wa mtu**

Ama kuhus mtu ambae Ramadhaan imemuingilia lakini akawa yeye hajui, basi akala na akanywa, mtu kama huyo na ajizuiye kula na kunywa na akamilishe saumu yake pindi atakapojua (yakwamba ni Ramadhaan) – na inahesabiwa kwake. Ama kwa yule ambae hajakula chochote basi na asile kitu, na kuwa na niya tangu jana usiku si sharuti kulingana na hali yake kwa sababu hawezi kufanya hivyo, na mojawapo ya misingi maarufu ya Sharee'ah ni kwamba uwajibikaji na mahitaji hutegemea juu ya uwezo wa mtu.

'Aa'isha ((رضي الله عنها amesema: *"Alikuwa Rasoolullaah ((صلى الله عليه وسلم akituamrisha kufunga katika siku ya 'Aashooraa', ilipofaradhishwa Ramadhaan ilikuwa katika hali yakwamba atakae na afunge, na atakae asifunge [siku hiyo]."*

Kutoka kwa Salamah Ibn al-Akwa' (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume *(صلى الله عليه وسلم)alimuamrisha mtu kutoka kabila la Aslam kuwalingania watu yakwamba yoyote aliyekula, basi na afunge katika wakati uliobaki, na yoyote ambaye hajakula kitu – basi na aendelee kufunga, kwa sababu hiyo ni siku ya 'Aashooraa'*

Kwahivyo siku hii ya 'Aashooraa' ilikuwa ni faradhi, kisha (baadae) uwajibu wake ukafutwa (ukaodolewa) – na wameamrishwa kuwacha kula wakati wa mchana na hilo likawatosha, na Ramadhaan ni waajib, na hukmu ya kitendo cha faradhi haibadiliki.

- **Baadhi ya wanavyuoni wamekataa na kusema yakwamba mtu kama huyo itamlazimu ailipe saumu hiyo baadae**

Baadhi ya wanavyuoni wameshikilia yakwamba kufunga saumu ya 'Aashooraa' haikuwa ni faradhi. Lakini fahamu, Ewe ndugu yangu katika eemaan, yakwamba dalili zinapochukuliwa kwa pamoja zinaonyesha yakwamba kwa hakika saumu ya 'Aashooraa' ilikuwa imefaradhishwa. Hii imethibitishwa kulingana na jinsi amri ilivyoafikiana katika hadeeth ya 'Aa'ishah.

[Endelea kwenye Makala Yajayo]

Siddiq Hassan Khan (rahimaullah)[14] akasema: "Mwezi kongo utakaposhuhudiwa na watu katika kitongoji chochote, basi itawapasa watu wote wakubaliane kuhusu kuonekana kwa mwezi huo. Ushahidi unatokamana na hadithi zinazoeleza kuhusu kuanza na kumaliza kufunga kwa kuuona mwezi kongo. Hadithi hizi zawaeleza Umma mzima wa waislamu: Muislamu yoyote akiushuhudia mwezi popote, ushuhuda wake utakuwa ni ushuhuda wa waislamu wote. Itakuwa ni makosa kwenda kinyume na hivi kwa kuitumia hadithi ya Kurayb (sahih Muslim) kwa sababu Ibn 'Abbas kwenye hadithi hiyo hakukatazwa na mtume (s.a.w.) kufuata utazamaji wa sehemu nyingine za mji."[15] Kuhusu mas-ala haya, akaeleza mwanachuoni wa karne hii, Muhammad Nasir Ud-Din Al-Albaani, (Rahimahullah): "Matla' zinahusiana wala hazina mipaka maalum ambayo watu waweza kuyatafautisha ili wazitegemee... wanavyuoni wengi hawakuyapa uzito mas-ala hayo ya tafauti za matla'. Ushahidi ukapatikana kutokamana na hadithi iliyosahih, 'Fungeni kwa kuuona na fungueni kwa kuuona.' Huu ndio ukweli uliothubutu, wala mtu asiupinge ukweli huu kwa kuitumia hadithi ya Ibn 'Abbas, huwenda ikawa ni bora kusema yakwamba hadithi ya Ibn 'Abbas inawahusu waliofunga kwa kuuona mwezi kwenye sehemu yao na baadae wakati wa Ramadhani wakajuwa ya kwamba mwezi kongo ulionekana mahali pengine siku moja kabla. Katika hali hiyo, watu hao wataendelea kufunga na wenzao kwenye sehemu yao mpaka wakamilishe siku thalathini au wauone mwezi wao. Jambo hilo litaondoa kutatizika na hadithi ifahamike kwa watu wote watakaofikiwa na habari za kuandama kwa mwezi kutoka sehemu yoyote. Ni wazi ya kwamba mas-ala haya ni rahisi kuyatekeleza siku hizi."[16]

KWA MUKHTASAR:

Ufuatao ni mukhtasar wa maelezo yaliopita:

a. Kuanza kwa mwezi wa ki-islamu hutegemea (kwa min-ajil ya kufunga, Hija na matukio mengine ya ki-islamu). Kuuona mwezi kongo kwa macho makavu.

b. Ushahidi wa utaalamu wa elimu ya nyota haufai kutumiwa katika kuthibitisha, kuhakikisha na wala kumkanusha muislamu muaminifu alieuona mwezi.

c. Pindi mwezi kongo uonekanapo popote ulimwenguni itawapasa watu wengine wote kufunga, maadamu habari zitawafikia ndani ya muda ambao watakuwa wepesi wa utekelezaji. Watu wasiowajibika kutekeleza amri hiyo ni waislamu wanaoishi chini ya mamlaka ya serikali inayokanusha (kwa masikitiko), kwa sababu mbalimbali, kufuata kuonekana kwa mwezi kutoka nchi nyengine.

d. Mwanzo wa mwezi ni kuonekana kwa mwezi kongo, bila ya kujali iwapo mwezi huo uliandama kabla, baada ama ndio umejitokeza wakati huo. Kwa hayo tunamuomba Allah (s.w.t.) atuongoze na atuwezeshe kuifuata Sunnah wakati wowote na mwito wetu wa mwisho uwe ni: AL-HAMDU LILLAHI RABBIL 'ALAMIN.

Ukumbi Wa Wanawake

...Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-Uthaymeen] (رحمه الله)

(Endelea kutoka Volume1, Issue 2)

a)**Talaka:** Inajulikana yakwamba kumpa talaka mwanamke asiyekuwa na mimba ni lazima iwe katika *Eda* yake (yaani: katika hali yake ya twahara ambayo mumewe hajamuingilia au iwapo imejulikana yakwamba tayari ashabeba mimba) na wala sio akiwa katika heidh yake kwa sababu kulingana na sheriya ya ki-Islamu ni Haramu.

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema:

"Munapowaacha wanawake, wawacheni wakiwa katika Idda zao."

Kadiri ya uhusiano alonao mwanamke mwenye mimba anavyohusika, Idda yake ni ule muda wake wa kuhimili mimba, awe na heidh au laa. Kwahivyo, talaka yake itategemea kukamilika muda wake wa mimba na wala haina uhusiano wowote na heidh yake.

b)Idda ya mwanamke mwenye mimba humalizika na mazazi yake, awe na heidh au laa, kutokana na maneno yake Allaah (سبحانه وتعالى):

"Kwa wale wenye mimba (Emma wawe wameachwa au wamefiliwa na waume zao), muda wao ni mpaka watakapozaa."

Mabadiliko Katika Hali Za Heidh

Kuna aina nyingi za mabadiliko zenye kuathiri hali za heidh:

Ya Kwanza: Kuzidi au kupungua, kwa mfano, muda ambao kwa kawaida huchukuwa siku sita huongezeka kwa siku moja zaidi au muda ambao kwa kawaida huchukuwa siku saba hupungua kwa siku moja na kumalizikia katika siku ya sita.

Ya Pili: Kutangulia au Kuchelewa, Kwa mfano, mwanamke mwenye kuipata heidh yake "ya kawaida" kila ifikapo mwisho wa mwezi akajiona heidh imemuingilia mwanzoni mwa mwezi au kinyume chake. Wanavyuoni wamekhitilafiana kuhusu hukmu ya kisheriya inayohusiana na hali hizi mbili.

Msimamo wa sawa ni kwamba kila mwanamke aonapo damu basi hiyo huwa ni heidh na kila anapotwahirika basi huwa yuko katika hali ya usafi, bila ya kujali iwapo kumetokea nyongeza, upungufu, kutangulia au kuchelewa katika heidh yake. Hii ni kwa sababu kuwajibika kwa hukmu za heidh, kama tulivyotangulia kuzitaja, hutegemea juu ya uhakika wa kupatikana damu ya heidh.

Ya Tatu: Kutokwa na chepechepe yenye rangi ya manjano (kama usaha wa manjano) au *Kurdah*: mithili yake ni baina ya mturuziko wenye rangi ya manjano na nyeusi. Itokeapo hali hiyo wakati wa muda wa heidh au punde tu imalizikapo na kabla ya kuwa katika hali ya twahara (kutwahirika), basi itazingatiwa kuwa ni heidh na kuwajibika chini ya hukmu za heidh. Ikiwa mituruziko hiyo itatokea baada ya hali ya twahara, basi hiyo si heidh kutokana na hadeeth iliyopokewa na Abu Daawud kutoka kwa Umm 'Atiyyah ((رضي الله عنها aliposema:

"Hatukuzingatia chepechepe ya manjano baada ya kutwahirika kuwa na umuhimu wowote (kuhusiana na heidh)."

Nae Imaam al-Bukhaari vilevile akapokea hadeeth kama hiyo bila ya maneno "baada ya kutwahirika".

"Hatukuzingatia chepechepe ya manjano kuwa na umuhimu wowote kuhusiana na heidh."

Hata hivyo, Imaam al-Bukhaari akaiorodhesha hadeeth hii chini ya mlango:

Mlango: Kumuhusu mwanamke atakaeona majimaji yenye rangi ya manjano baada ya kutwahirika."

Aliiegemeza hadeeth hii juu ya hadeeth nyengine iliyopokewa na 'Aaisha kwenye mlango huohuo kwa jina la **"Mwanzo na mwisho wa heidh"**:

"Na walikuwa wanawake wakipeleka pamba zikiwa na alama za mituruziko ya manjano kwa 'Aaisha ((رضي الله عنهما (kwa kutaka kujua hukmu zao iwapo wameshatwahirika kutokamana na heidh au laa), na 'Aaisha alikuwa akiwaambia, "musifanye haraka mpaka muone Al-Qassatal' Baydhaa' (mturuziko mweupe kutoka katika kizazi; Pamba hizo zitakuwa nyeupe) kumaanisha kumalizika kikamilifu kwa heidh."

Ya Nne: Kukatika kwa heidh kiasi cha kwamba damu hutoka siku moja na kusimama siku ifuatayo. Kuna hali mbili zinazohusiana na mas'ala haya:

a) Kukatika huku kwa damu hutokea mara kwa mara. Katika hali hii damu hii huzingatiwa kuwa ni damu ya Istihaadhah na hukmu zote za Istihaadhah zinapasa kuwajibika hapa.

b) Kukatika kwa damu hutokea mara nyengine na hupatikana muda wa kutwahirika. Wanavyuoni wamekhitilafiana hapa kuhusu muda huu wa kutwahirika: jee, huu kweli ni muda wa twahara, hali ambayo hukmu za heidh haziwajibiki, au ni katika sehemu ya heidh?

Kulingana na madh-hab za Imaam ash-Shaafi'ee, Ibn Taymiyyah, na Imaam Abu Haneefah, muda huu wa mjumuiko ni katika sehemu ya heidh, kwa sababu Qassah Al-Baydhaa' haionekani na iwapo itazingatiwa kuwa ni "Twahara" basi kutakuwa na uzito na taklifu juu ya wanawake. Kwa hakika, hayo ni kinyume cha misingi asili ya ki-Islamu.

Kwa upande mwengine, rai iliyo mashuhuri ya madh-hab ya ki-Hanbali ni kwamba damu itokayo ni heidh na kutakasika ndiyo "twahara" isipokuwa ikiwa nyakati za heidh na twahara kwa pamoja zitapita "muda mrefu zaidi wa heidh" ambao kulingana na madh-hab hii ni siku kumi na tano. Damu hutoka kupita "kiwango cha juu" huzingatiwa kuwa ni *Istihaadhah*." Muandishi wa *Al-Mughnee* (kitabu kikubwa cha maregeo kilichokusanya Fiqh ya madh-hab ya ki-Hanbali) amesema:

"Iwapo damu itasimama kwa muda usiozidi siku moja, hali hiyo haitozingatiwa kuwa ni "Twahara" isipokuwa kama ataona ushahidi wa wazi, kwa mfano, damu ikisimama mwishoni mwa ada yake au akaiona Qassah Al-Baydhaa'"

Muandishi huyu akasema: "Maneno hayo ya katika Mughnee ni msimamo wa kati na kati baina ya rai mbili zilizotangulia, na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi wa hayo."

Ya Tano: Ukavu ndani ya damu: Mwanamke akiona anatokwa na chepechepe iliyorowama. Yakitokea hayo wakati akiwa kwenye heidh au kuhusiana nayo, kabla ya "Twahara", basi hiyo itakuwa ni heidh. Na iwapo itatokea baada ya twahara, basi hiyo haitokuwa heidh.

Hukmu Kuhusiana Na Heidh

Kuna hukmu nyingi zenye kuhusiana na heidh. Inatosheleza kutaja zile zenye kuhitajika zaidi.

Ya Kwanza: Heidh na Swala .

Aina zote za Swala, za waajib au Sunnah zimeharamishwa kwa wanawake wakiwa kwenye ada zao. Haimpasi mwanamke kuswali isipokuwa iwapo ataweza kupata rakaa'ah kwa ukamilifu ndani ya wakati ulioamrishwa wa swala. Kwa ufafanuzi wa hayo utafakari mfano ufuatao:

(Endelea Kwenye Makala Yajayo)

P. O. Box 85477,
Mombasa,

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفرقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net